

Tangazo La Serikali Na 530 La Tarehe 10/7/2020

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA. 290)

**SHERIA NDOGO**

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7 (1) (g) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO) (MAREKEBISHO) HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI ZA MWAKA 2020

- |  |   |
|--|---|
| Jina la Sheria   | 1. Sheria Ndogo hii zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, za mwaka 2020 na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi (Ushuru wa Mazao) za mwaka 2008 ambazo zitajulikana kama Sheria Ndogo Kuu.   |
| Marekebisho ya Tangazo Na 237 ya tarehe 24/10/2008<br>Marekebisho ya Tangazo Na 237 ya tarehe 24/10/2008 | 2. Marekebisho yanafanyika katika kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo Kuu kwa kubadilisha viwango vya ushuru katika Jedwali la Kwanza Sehemu "A".<br>3. Marekebisho yanafanyika katika kifungu cha 13 (1) cha Sheria Ndogo Kuu kwa kukifuta na kukiandika upya na sasa kitasomeka Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria Ndogo hii atakua ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa kiasi kisichopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na kisichoziidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichoziidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja. |
| Kufililisha Kosa   | 4. Marekebisho yanafanyika kwa katika Sheria Ndogo Kuu kwa kuongeza kifungu kipya cha kufililisha kosa ambacho kitasomeka "Bila kujali masharti ya Sheria Ndogo hii, Mkurugenzi anaweza kufililisha kosa kwa kutoza kiasi cha shilingi laki mbili kwa mtu yeyote atakayekiri kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii na kuwa tayari kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii."  |

*Sheria Ndogo Za (Ushuru wa Mazao) (Marekebicho) Halmashauri ya Wilaya Ya Moshi*

*Tangazo la Serikali Na. 530 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 2)*

SEHEMU "A"

Na.	Aina ya mazao	Kiasi cha ushuru unaotozwa
1.	Kahawa	3% ya bei ya mauzo
2.	Maharage	3% ya bei ya mauzo
3.	Nyanya	3% ya bei ya mauzo
	Vitunguu	3% ya bei ya mauzo
	Viazi	3% ya bei ya mauzo
4.	Mchele	3% ya bei ya mauzo
5.	Maparachichi	3% ya bei ya mauzo
6.	Ndizi	3% ya bei ya mauzo
7.	Maua	3% ya bei ya mauzo
8.	Mahindi	3% ya bei ya mauzo
9.	Miwa	3% ya bei ya mauzo

JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 4)*  
HATI YA KUFILILISHA KOSA

Mimi ..... nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya..... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwamba tarehe .....ya Mwezi ..... Mwaka..... nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ..... cha Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Mazao (Marekebicho) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi za Mwaka 2020.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi ninachodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe .....ya Mwezi .....Mwaka .....

Jina: .....

Saini: .....

Mbele ya:

Jina.....

Cheo: .....

Saini: .....

Tarehe: .....

*Sheria Ndogo Za (Ushuru wa Mazao) (Marekebicho) Halmashauri ya Wilaya Ya Moshi*

*Tangazo la Serikali Na. 530 (Linaendelea.)*

---

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imebandikwa katika Sheria Ndogo hizi kwa Azimio la kikao cha Halmashauri kilichoitishwa na kufanyika tarehe 29/2/2019.

KASTORI G. MSIGALA,  
*Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya,  
Moshi*

MHE. MICHAEL S. KILAWILA,  
*Mwenyekiti,  
Halmashauri ya Wilaya,  
Moshi*

NAKUBALI,



Dodoma,  
27 Desemba, 2019

MHE. SELEMANI S JAFU (MB.),  
*Waziri-OR-Tamisemi*